**TAMKO LA KUWAPONGEZA VIONGOZI WA SERIKALI WANAOHIMIZA UTAWALA WA SHERIA NA UTAWALA BORA NCHINI**

**Utangulizi**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) kwa mara kadhaa umekuwa na unaendelea kutoa wito kupitia matamko mbali mbali kuwataka viongozi wa umma hususani wakuu wa wilaya na mikoa kuacha tabia ya kutoa amri za kuwaweka watu ndani bila sababu za msingi. Mtandao pia umekuwa ukitoa wito katika mikutano na warsha mbali mbali kati yake, wanachama na viongozi mbali mbali wa serikali. Muendelezo wa kukemea amri za wakuu wa mikoa na wilaya hapa nchini unatokana na Sheria ambazo tumekuwa tukipigania zifanyiwe mabadiliko.

**Pongezi kwa Viongozi wa Serikali Wanaohimiza Utawala wa Sheria na Utawala Bora Nchini**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu unapenda kutoa pongezi kwa Waziri katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) Suleiman Jafo pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Mhandisi Musa Iyembo ambao wakati wa mafunzo kwa wakuu wapya wa Wilaya na Wakurugenzi waliwaonya kutokujichukulia sheria mkononi kwa kutoa amri za kuwaweka ndani baadhi ya watu wakiwemo watumishi wa umma, viongozi na watetezi wa haki za binadamu kinyume na misingi ya haki za binadamu, utawala wa sheria za na Katiba ya Tanzania .

Kitendo cha Waziri wa Ofisi ya Rais TAMISEMI na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kusimama na kukemea tabia hii ni mfano mzuri wa viongozi bora na wanastahili kupongezwa na watanzania wote. Ni wazi kwamba viongozi wa juu wasiposimama na kuwaonya au kuwashauri viongozi wa chini yao Taifa litashindwa kwenda katika njia ya mfumo wa utawala bora wenye kuheshimu haki za binadamu. Mfano huu unapaswa kuigwa na viogozi wengine wa juu serikaliini hasa vyombo vile vinavyosimamamia maadili ya uongozi, tawala za mikoa, usalama wa raia, utawala bora na haki za binadamu. Ikumbukwe kuwa Mhe Rais hawezi kukemea au kuonya kila kiongozi au mtumishi wa umma ila anaweza fanya hivyo kupitia viongozi wake wakuu kama

mawaziri, viongozi wa taasisi kubwa za Taifa kama Jeshi, Polisi ,Mahakama, Bunge, Tume ya Haki za Binadamu na hata viongozi wakuu wa chama tawala. Hivyo walichofanya Waziri wa Tamisemi na Katibu wake ni heshima kubwa kwa Ofisi ya Rais na inaleta picha nzuri kwa wananchi na mahusiano mazuri kati ya wateule wa Rais na wananchi waliomchagua Rais.

Kipekee pia tunapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk John Joseph Pombe Magufuli kwa kupokea ushauri wa viongozi wanaomzunguka na kuwaondoa baadhi ya viongozi wasiokuwa waadilifu na kuteua viongozi wapya kwa ajili ya kuhakikisha utawala wa sheria, misingi ya haki za binadamu na maendeleo ya taifa letu kwa ujumla.

Amri zinazotolewa na wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa mbali mbali Tanzania bila kuwa na sababu za msingi imekuwa ni moja ya sababu ya wananchi wakati mwingine kuanza kuichukia serikali na viongozi wake kwani wakuu wa wilaya na mikoa wamekuwa wakiagiza kukamatwa na kuwekwa ndani wananchi kwa masaa 48 bila hatia na baadae wanashindwa kuwafungulia mashtaka kwakuwa amri hizo mara nyingi zinatolewa wakati mwingine bila hatia. Tunaamini kwamba viongozi hawa wanasimamia na kuwaongoza wananchi kwa niaba ya Rais, lakini majukumu yao wanatakiwa kuyatekeleza kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi bila kuonea mtu au kuvunja haki zao. Hata hivyo, viongozi wanaomuwakilisha Rais wamekuwa wakikiuka misingi ya haki na sheria kwa kutoa amri zinazoenda kinyume kabisa na majukumu yao kisheria, utawala bora na haki za haki za Binadamu.

Katika hatua nyingine, tunampongeza Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. William Lukuvi kwa kuondoa kodi ya ardhi kwa taasisi zinazofanya kazi za kijamii bila kujiingizia faida yoyote. Tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo, taasisi zinazofanya kazi za kijamii hasa asasi za kiaraia zitapata motisha na kuweza kujitanua na kufikia watu/jamii kubwa zaidi na hivyo kuisaidia serikali katika kutoa huduma mbali mbali za jamii.

Pia tunampongeza Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Philip Mpango ambaye katika Bunge la Bajeti ya Mwaka huu alichukua uamuzi wa kufuta kodi ya taulo za kike (Pedi) jambo ambalo litasaidia waschana wengi na wanawake ambao kwa namna moja ama nyingine walikuwa wanashindwa kumudu gharama hizo.

Ikumbukwe kwamba taasisi zetu hasa zile zinazotoa huduma kwa jamii kama asasi za kiraia zinapata misaada ya walipa kodi wa nchi zingine kwa lengo la kusaidia watanzania hivyo hivyo si busara tena kuweka kodi kwenye misaada inayokwenda kwa wanachi.

**Wito wetu kwa Viongozi wengine wa Serikali:**

- Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unatoa wito kwa viongozi wengine kuiga mwenendo wa viongozi tajwa hapo juu ili kuhakikisha kwamba haki, utii wa sheria, demokrasia na maendeleo ya nchi vinadumishwa kwa manufaa ya kizazi cha leo na kesho.
- Pamoja na kwamba tunasisitiza kwamba viongozi wa wilaya na mikoa wanatakiwa kutotoa amri za kuwakamata watu bila hatia, tunashauri pia kwamba ingekuwa vyema Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 1997 baadhi ya vifungu vifanyiwe marekebisho kwani vinatumiwa vibaya na baadhi ya viongozi.
- Kuhusu msamaha wa kodi, tunawaomba viongozi hususani Kamishna wa TRA na Waziri wa Fenda na Mipango kutoa msamaha wa baadhi ya kodi kwa Asasi za Kiraia ili zipanue wigo wa kazi zao katika kuisaidia kutoa huduma mbalimbali za jamii.
- Tunashauri Vionngozi wote wenye mamlaka ya juu wasisite kukemea viongozi wa chini wanaonekana kwenda kinyume na utawala wa sheria na misingi ya utawala bora.

**Mwisho:**

Tunalazimika kuyasema haya kwakuwa mbali na kwamba amri hizo zinasababisha wananchi kuichukia serikali yao na viongozi, pia wahanga wa amri hizo wanapata adha pale wanapowekwa ndani na baadae kuachiliwa bila hatua zozote kuchukuliwa. Aidha, sisi kama Mtwandao pia tumekuwa tukiingia gharama kubwa za kuweka mawakili wa kusimamia kesi za watetezi wanaokuwa wahanga wa amri za wakuu wa wilaya na mikoa. Fedha tunazopoteza zingeweza zikatumika kusaidia katika kazi zingine za ustawi wa jamii yetu. Mpaka sasa Mtandao umesimamia kesi zaidi ya 4 ambazo zimetokana na amri za wakuu wa Wilaya/Mikoa.

Kama Mtandao tumeona ni vyema kupongeza juhudi na kauli hizi za baadhi ya viongozi wetu kwakuwa zinatia moyo na zinaonyesha kuwa baadhi ya viongozi wamekuwa wasikivu na wanayafanyia kazi yale ambayo wananchi wamekuwa wakilalamikia kwa muda mrefu.

**Imetolewa leo tarehe 17/08/2018**

**Na**

**……………………………….**

**Onesmo Olengurumwa**

**Mratibu, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**